



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE



TANGAZO LA ZABUNI YA KUWAPATA MAFUNDI WA UJENZI KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE

06/12/20222

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE ANAWATANGAZIA WANANCHI KUHUSU ZABUNI YA KUWAPATA MAFUNDI WA UJENZI WA NYUMBA MBILI ZA WATUMISHI KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE.

Hivyo mafundi wanatakiwa kuwa na nguvu kazi ya kutosha kuweza kukamilisha kazi kwa wakati, Mwajiri hataongeza muda kwa fundi yoyote ataechelewa kufikia lengo.

1. SIFA ZA MAFUNDI WANAOHITAJIKA

- Ajue kusoma na kuandika kwa lugha ya Kiswahili kwa ajili ya mawasiliano ya maandishi.
- Fundi awe na namba ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN).
- Fundi awe tayari kulipwa kulingana na taratibu za malipo ya kiserikali hivyo ni lazima awe na Akaunti ya malipo kutoka Benki inayotambulika hapa Nchini kama vile NMB, CRDB na kadhalika kwakuwa malipo yatafanyika kupitia Benki na ahakikishe anatumia jina ambalo lipo kwenye Akaunti yake ya Benki.
- Fundi anatakiwa kuelewa kwamba hakutakuwa na malipo ya awali (advance), Fundi atatakiwa kuanza sehemu ya kazi ndipo aombe malipo kulingana na kazi aliyofanya.
- Fundi awe tayari kufuata maelekezo ya Mhandisi Mshauri wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe katika kutekeleza kazi ya Mradi.
- Fundi atatakiwa kutaja gharama ya kazi yote kulingana na Mchoro ikihusisha ujenzi wa Jengo.
- Fundi awe na uzoefu usiopungua miaka mitatu (3) na uthibitisho wa kazi alizowahi kuzifanya kwa barua kutoka kwa mwajiri au Taasisi yoyote ya umma au binafsi. Fundi mwenye cheti cha VETA atapewa kipaumbele.

2. MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA ZABUNI HII

- 1) Fundi anaruhusiwa kutembelea eneo la kazi ili kujionea uhalisia wa kazi kabla ya kuleta zabuni yake.
- 2) Halmashauri itanunua vifaa vyote vitakavyoitajika katika Ujenzi.
- 3) Fundi atapewa vifaa kulingana na kazi anayofanya na atawajibika kisheria kwa matumizi mabaya ya vifaa katika utekelezaji wa Mradi.
- 4) Fundi atakayebainika kuiba vifaa vya Ujenzi atakuwa amejifukuzisha mwenywe na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.
- 5) Fundi atafanya kazi kwa kufuata maelekezo ya Mhandisi wa Halmashauri katika kutekeleza mradi.
- 6) Ada ya maombi ya zabuni hii ni Tsh. 20,000/= ambayo italipwa kwa kutumia control namba utakayopewa na Ofisi ya Wahasibu.
- 7) Maombi ya Zabuni yawasilishwe kwa mkono katika bahasha iliyofungwa vizuri yakiwa na risiti ya ada ya zabuni kiasi cha 20,000/=, Maombi yatakawasilishwa kwa njia nyingine hayatasomwa siku ya ufunguzi na hivyo hayatafanyiwa kazi.
- 8) Michoro na Schedule of Labour zitapatika Ofisi ya Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi baada ya kulipa Ada ya Zabuni.
- 9) Maombi yaoneshe Jina kamili la mwombaji wa zabuni, anuani pamoja na namba ya simu na yatumwe kwa:

**MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE,
S. L. P 77,
MKWAJUNI- SONGWE.**

Mwisho wa kupokea maombi ni siku ni TAREHE 13 DISEMBA 2022 saa 8:00 mchana. Zabuni zote zitafunguliwa hadharani mbele ya Mafundi au Wananchi amabo watapenda kuhudhuria katika ufunguzi wa zabuni. Zabuni itakayochelewa kuwasilishwa katika siku ya ufunguzi katika muda uliotajwa haitafunguliwa.



**CPA CECILIA D. KAVISHE
MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
SONGWE**